JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

TAARIFA YA MHESHIMIWA JAJI WA RUFANI JACOBS C. M. MWAMBEGELE MWENYEKITI WA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI KWA UMMA KUHUSU UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA AWAMU YA PILI NA UWEKAJI WAZI WA DAFTARI LA AWALI LA WAPIGA KURA

Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Ndugu wananchi!!

1.0. UTANGULIZI

Kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 16(5) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya mwaka 2024, Tume inao wajibu wa kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mara mbili mara baada ya uchaguzi mkuu na kabla ya uteuzi wa wagombea kwa uchaguzi mkuu unaofuata.

Katika utekelezaji wa kifungu hicho, Tume iliboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura awamu ya kwanza kuanzia tarehe 20 Julai, 2024 na kukamilisha tarehe 25 Machi, 2025.

Hivyo, Tume inawapongeza wananchi wote waliojitokeza kwa wingi nchi nzima kujiandikisha kwa mara ya kwanza, kuboresha au kuhamisha taarifa zao na kupata kadi mpya kwa wale ambao kadi zao zimepotea au zimeharibika.

2.0. MIZUNGUKO YA UBORESHAJI WA DAFTARI LA WAPIGA KURA AWAMU YA PILI

Ndugu wananchi!!

Kama nilivyorejea kifungu cha 16(5) cha Sheria tajwa, Tume imekamilisha maandalizi ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura awamu ya pili.

Hivyo, napenda kutoa taarifa rasmi kwamba, zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura awamu ya pili litafanyika kuanzia tarehe 01 Mei, 2025 hadi tarehe 04 Julai, 2025.

Uboreshaji huu utakuwa katika mizunguko mitatu kama ifuatavyo:

2.1. Mzunguko wa Kwanza.

Mzunguko wa kwanza wa zoezi la uboreshaji wa Daftari awamu ya pili utahusisha mikoa 15 kwa wakati mmoja na utafanyika kwa muda wa siku saba kuanzia tarehe 01 Mei, 2025 hadi tarehe 07 Mei, 2025 ambapo vituo vya uandikishaji 3,808 vitatumika.

Mikoa itakayohusika katika mzunguko wa kwanza ni; Geita, Kagera, Mara, Shinyanga, Mwanza, Simiyu, Rukwa, Tabora na Katavi. Mikoa mingine ni Kigoma, Iringa, Ruvuma, Mbeya, Njombe na Songwe.

2.2. Mzunguko wa Pili.

Mzunguko wa pili wa zoezi la uboreshaji wa Daftari awamu ya pili utahusisha mikoa 16 kwa wakati mmoja na utafanyika kwa muda wa siku saba kuanzia tarehe 16 Mei, 2025 hadi tarehe 22 Mei, 2025 ambapo vituo 3,921 vitatumika.

Mikoa itakayohusika katika mzunguko wa pili ni; Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro, Pwani, Singida, Dodoma na Dar es Salaam. Mikoa mingine ni Lindi, Mtwara, Mjini Magharibi, Kaskazini Unguja, Kusini Unguja, Kaskazini Pemba na Kusini Pemba.

2.3. Mzunguko wa Tatu

Mzunguko wa tatu wa zoezi la uboreshaji wa Daftari utahusisha vituo 130 vilivyopo kwenye magereza ya Tanzania Bara na vituo 10 vilivyopo katika Vyuo vya Mafunzo Tanzania Zanzibar kwa wakati mmoja na utafanyika kwa muda wa siku saba kuanzia tarehe 28 Juni, 2025 hadi tarehe 04 Julai, 2025.

Ndugu wananchi!!

Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa awamu ya pili, utafanyika ngazi ya kata kwa Tanzania Bara na ngazi ya jimbo kwa Tanzania Zanzibar, ambapo jumla ya vituo 7,869 vitahusika, vituo 7,659 vipo Tanzania Bara na vituo 210 vipo Tanzania Zanzibar.

Aidha, tunatarajia kuwa katika awamu ya pili ya uboreshaji, wapiga kura wapya **1,396,609** wataandikishwa, wapiga kura **1,092,383** wataboresha taarifa zao na wapiga kura **148,624** watafutwa kwenye Daftari kwa kukosa sifa za kuendelea kuwepo kwenye Daftari.

Ndugu wananchi!!

Uboreshaji wa Daftari utahusisha mambo yafuatayo; -

(i) kuandikisha wapiga kura wapya ambao ni raia wa Tanzania wenye umri wa miaka 18 na zaidi na watakaotimiza umri huo ifikapo tarehe ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025;

(ii) kutoa kadi mpya kwa wapiga kura waliopoteza kadi au kadi zao kuharibika;

(iii) kutoa fursa kwa wapiga kura walioandikishwa kurekebisha taarifa zao yakiwemo majina na taarifa nyingine;

(iv) kuhamisha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka kata au jimbo walipoandikishwa awali; na

(v) kuondoa taarifa za wapiga kura waliopoteza sifa za kuwemo kwenye Daftari kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kifo.

Kama ilivyo kawaida, vituo vya kuandikisha wapiga kura vitafunguliwa saa 02:00 asubuhi na kufungwa saa 12:00 jioni.

Ndugu wananchi!!

Kila chama cha siasa kimepewa nakala ya orodha ya vituo vyote 7,869 vya kuandikisha wapiga kura vitakavyotumika kwenye uboreshaji wa Daftari kwa awamu ya pili.

Dhumuni la kuwapatia nakala hizo ni kuviwezesha kupanga na kuweka mawakala wa uandikishaji katika vituo vya kuandikisha wapiga kura.

Kila chama kitaruhusiwa kisheria kuweka wakala mmoja kwenye kituo cha kuandikisha wapiga kura kwa lengo la kushuhudia utekelezaji wa zoezi la uboreshaji kituoni ikiwemo kuwatambua wale wanaokuja kituoni kama wana sifa za kuandikishwa au la.

3.0. UWEKAJI WAZI WA DAFTARI LA AWALI LA WAPIGA KURA KWA AJILI YA KUKAGULIWA NA UMMA

Ndugu wananchi!!

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 11(1) na (2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, Tume

pia ina jukumu la kuandaa Daftari la Awali la Wapiga Kura na kuliweka wazi kwa umma.

Lengo la uwekaji wazi wa Daftari hilo ni kutoa fursa kwa wananchi kukagua, kufanya marekebisho ya taarifa za wapiga kura na uwekaji wa pingamizi dhidi ya wapiga kura waliomo kwenye daftari ambao hawana sifa.

Daftari la Awali la Wapiga Kura litabandikwa katika vituo vyote vilivyotumika wakati wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura awamu ya kwanza na utaratibu utakaotumika kwa wapiga kura kuhakiki taarifa zao ni kwa;-

(i) mpiga kura mwenyewe kufika katika kituo alichojiandikisha na kuhakiki taarifa zake katika orodha itakayokuwa imebandikwa katika kituo hicho;

(ii) mpiga kura kupitia simu yake ya kiganjani kupiga namba *152*00# na kufuata maelekezo yatakayomwezesha kuhakiki taarifa zake;

(iii) mpiga kura kupiga simu namba 0800112100 na kupewa maelekezo yatakayomwezesha kuhakiki taarifa zake; na

(iv) mpiga kura kuhakiki taarifa zake kupitia Tovuti ya Tume, www.inec.go.tz kwa kubonyeza sehemu iliyoandikwa 'uhakiki' na kuendelea kufuata maelekezo.

Aidha, iwapo mpiga kura atahitaji kuboresha taarifa zake au kuweka pingamizi dhidi ya mpiga kura asiye na sifa za kuwemo kwenye Daftari la Awali la Wapiga Kura ataenda katika kituo kilichopangwa kwenye kila kata katika halmashauri husika kuweka pingamizi au kuboresha taarifa zake.

Hivyo, zoezi hili la uwekaji wazi wa Daftari la Awali la Wapiga Kura litafanyika pamoja na uboreshaji wa Daftari wa awamu ya pili.

4.0. HITIMISHO

Ndugu wananchi!!

Napenda kutumia fursa hii kusisitiza kuwa, mawakala au viongozi wa vyama vya siasa hawaruhusiwi kuingilia mchakato wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kituoni.

Hivyo, niwaombe viongozi wa vyama vya siasa na wadau wa uchaguzi kwa ujumla kuzingatia sheria ya uchaguzi, kanuni za uboreshaji, maelekezo ya Tume na kusimamia miiko na mipaka ya uendeshaji wa zoezi la uboreshaji wa Daftari.

Ndugu wananchi!!

Kwa kumalizia, napenda kutoa wito kwa wananchi wote wenye sifa kujitokeza kwa wingi na kutoa ushirikiano kwa Tume wakati wote wa utekelezaji wa jukumu hili muhimu kwa mustakabali wa nchi yetu.

KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza

Jaji (Rufani) Jacobs C. M. Mwambegele
MWENYEKITI
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI
14 Aprili, 2025